Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Waambie waaminio wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; Bila shaka Allah Anazo habari za yale wanayoyafanya. Na waambie wanawake waaminio kwamba wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, na wasidhihirishe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa yale yaliyo bayana katika hayo, na kwamba washushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa kwa waume zao, au kwa baba zao au kwa baba za waume zao ... ... (23:31-32)

JUZU 78 No. 195 | RAMAD-SHAWW 1439 AH | JULAI 2018 | WAFA 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Watu Walio Bora Kabisa

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 01/06/2018, baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Hadhrat Ukasha bin Mesan ra, alikuwa sahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w anayehesabika kuwa miongoni mwa masahaba wakubwa. Yeye alishiriki vita vya Badri akiwa amepanda farasi. Siku hiyo upanga wake ulivunjika, hapo Mtukufu Mtume s.a.w akampatia mbao fulani iliyoonekana mkononi mwake kama ni upanga mkali sana wa chuma. Naye akapigana kwa upanga huo huo mpaka pale Mwenyezi Mungu Alipowajaalia ushindi.

Mtukufu Mtume s.a.w alikuwa amempatia habari njema alipomwambia: "Wewe utaingia peponi bila ya kufanyiwa hesabu." Wakati wa vita vya Badri, Mtukufu Mtume s.a.w aliwaambia masahaba ra ya kwamba: 'Leo mpanda farasi aliye bora kabisa miongoni mwa Waarabu yu pamoja nasi,



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

masahaba ra wakamwuliza: 'Ewe Mtume wa Allah, ni nani huyo?' Mtume s.a.w akasema: 'huyo ni Ukasha bin Mehsan.

Hadhrat Abu Hurairah r.a anasimulia ya kuwa, mimi nilimsikia Mtukufu Mtume s.a.w akisema ya kwamba, "miongoni mwa umma wangu lipo kundi moja litakaloingia peponi nalo litakuwa na watu elfu sabini ambao nyuso zao zitakuwa zikin'gaa kama mbalamwezi.

Hadhrat Abu Hureirah ra anasimulia ya kuwa, Hadhrat Ukasha bin Mehsan ra akasimama na akaipandisha juu shuka yake na kusema: "Ewe Mtume wa Allah s.a.w niombee kwa Mwenyezi Mungu Anijaalie niwe miongoni mwao." Mtukufu Mtume s.a.w akasema: "Ewe Allah Umjaalie huyu awe miongoni mwao." Hapo mtu mwingine miongoni mwa Maansar akasimama na kusema, "Ewe Mtume wa Allah s.a.w niombee kwa Mwenyezi Mungu ya kwamba Anijaalie mimi pia niwe miongoni mwao". Hapo Mtume s.a.w akasema: "SABAQAKA BIHAA UKASHA" yaani kuhusiana na hilo Ukasha amekutangulia".

Mtukufu Mtume s.a.w alimtuma Hadhrat Ukasha ra katika vita nyingi akiwa amemteua kuwa kiongozi wa jeshi. Katika mwezi wa Rabiul Awwal, mnamo mwaka wa sita wa Hijra, Mtume Mtukufu s.a.w alimtuma Hadhrat Ukasha ra akimteua kuwa kiongozi wa Waislamu

Endelea uk 2

Waziri wa Utawala Bora Asifu Islam Ahmadiyya Tanzania

Na **Seif Hassan Nakuchiima**
Dar es salaam

Waziri wa nchi ofisi ya Rais anaeshughulikia utumishi na utawala bora, George Huruma Mkuchika amepongeza Jamaat Ahmadiyya nchini kwa kudumisha amani. Mh. Mkuchika aliyasema hayo alipokutana na ujumbe wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania ulioongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry Sahib.

Mh. Mkuchika alisema kwa miaka takribani arobaini aliyofanya kazi Serikalini hajawahi kusikia Ahmadiyya ikijihusisha na mahubiri au mawaidha yenye kukashifu dini zingine au Serikali alisema. Amewahi kuhudumu nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala katika Mkoa wa Dar es Salaam kipindi ambacho wana dini wengi walikuwa wakitoa mihadhara yenye kukashifu dini na Serikali na hivyo kuhatarisha amani jambo ambalo Jumuiya ya Ahmadiyya kamwe na viongozi wake hawakushiriki aliongeza.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais wa Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa George Huruma Mkuchika akiwa na wageni wake nje ya ofisi ya wizara yake walioongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry

Mheshimiwa Mkuchika aliishukuru Jamaat Ahmadiyya Tanzania kwa kutekeleza miradi mbalimbali yenye kusaidia jamii ikiwa ni pamoja na maji, shule na hospitali. Alisema Serikali ina thamini sana taasisi za dini ambazo zinafanya kazi ya kuhudumia jamii na hivyo kusaidia juhudi za Serikali katika kutoa huduma na hasa pale ambapo Serikali hukumbana na changamoto za kukosa fedha aliendelea kusema.

Serikali inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuli imejikita katika kukusanya kodi ili iwe na wigo mpana wa utoaji wa huduma bora tena kwa wakati kwa wananchi. Mheshimwa Mkuchika alimsifu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa msimamo wake wa Serikali kutokuwa na dini na alisema ingawa jambo hili halikueleweka vizuri mwanzoni kwa sasa ni jambo linalosaidia sana katika kujenga amani, umoja na mshikamno wetu kwa kuwa kila mwananchi anapewa fursa ya kuhudumia nchi au kazi kwa kufuata vigezo vyake vya kufanya kazi na wala si katika misingi ya itikadi au dini alisema.

Waziri Mkuchika alitumia fursa hiyo kuwaomba viongozi wa dini kupitia Amir Sahib wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania kuendelea kuliombea Taifa letu na viongozi wake ili Mwenyezi Mungu Awape busara na hekima ya kuweza kuliongoza Taifa letu, alimalizia.

Aidha Mheshimiwa Waziri George Mkuchika, alionyesha kuifahamu Jumuiya ya Ahmadiyya kwa miaka mingi na anamkumbuka vizuri aliyekuwa Waziri wa kwanza Sheria na Katiba

Endelea uk 4

Islamu na Malezi Bora ya Watoto Uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Jihadhari Na Sala Ya Katikati

Kila zama na wakati. Vitu hivi viwili kwa shani ya ajabuvinadhihirisha kwa namna nyingine utukufu, usahihi wa Kitabu cha Allah Qurani Tukufu. Bila ya msaada wa Allah ni muhali kugusa kiini cha mafundisho ya Qurani Tukufu. Upo wakati maana za baadhi ya aya za Qurani Tukufu zinakuwa bayana zaidi.

Dunia yote kwa hivi sasa imegubikwa na ulevi. Ni ulevi ammbao unalewa bila kunywa chochote. Ni ulevi unaoamsha hisia kali. Ni ulevi unaoamsha uzalendo wa kufurutu ada. Ni ulevi wa watu kununiana na wasipeane hata salaam kwa muda. Ni ulevi unaomfanya mtu kulia machozi. Ni ulevi unaomfanya aongope na kutoa visingizio kwamba anaumwa ili muradi arudi nyumbani. Ni ulevi ambao magazeti yote yanazidhisha ulevi huo. Ni ulevi unaotawala luninga. Ni ulevi unaotawala mazungumzo yote. Kama hujagundua ulevi huo, ngoja tusaidiane. Ulevi huo na mchezo wa kabumbu kugombea Kombe la Dunia.



Islam inaheshimu sana michezo, tena michezo ya kila aina. Mpira ni mchezo mzuri tena una mafunzo tele. Unamarisha viungo, unajenga umoja na kuheshimiana, unakumbusha umuhimu wa ushirikiano. Unadhihirisha kidole kimoja hakivunji chawa. Unajenga uzalendo. Majuzi nilisikia shabiki mmoja akisema katu usiseme hiyo Nigeria hiyo ni Afrika. Ni dhahiri mpira una uwezo wa kufutilia kwa mbali fikra na hata ile mipaka iliyowekwa na mkoloni walipokutana katika jiji la Berlin 1884 Afrika ilipogawanywa kama wawindaji wanapogawana mnyama waliyemuua.

Kwa ujumla, tunnapenda na kuheshimu mchezo wa mpira. Na kama mafundisho ya Islam, daima tunatakiwa tuchukue njia ya kati. Njia ya wastani. Sote tunaelewa kwamba chumvi ni tamu lakini ikizidi inamchosha mlaji. Sukari ni tamu pia katika chai ikizidi inamkera mnywaji. Kama tulivyosema, mafunzo ya Islam ni kiasi. Wastwa. Kimsingi, wema na mahali pake. Mashindano ya mpira ya kugombea Kombe la Dunia usikubali kukusahaulisha shabaha ya kuumbwa kwako ambako ni kumwabudu Mwenyezi Mungu. Ukikubali hilo lifanyike basi utatukumbusha mshale ambao umepotelea msituni. Kombe la mpira la dunia lisikughafirishe na hotuba muhimu ya Ijumaa inayotolewa na Khalifatul Masih V a.t.b.a. Hakuna kitu cha muhimu kwa muaminio kwa hivi sasa kama kusikiliza na tena kusikiliza kwa amkini hotuba ya Ijumaa ya Khalifatul Masih. Ni jukumu la wazazi kuhakikisha ya kwamba watoto nao wanashiriki pia katika kusikiliza hotuba ya Khalifatul Masih. Ni njia ya kati tu basi itakayotuwezesha kupata shabaha ya kuumbwa kwetu.

Watu Walio Bora Kabisa

Kutoka uk. 1

arobaini ili kupigana na kabila la Bani Asad. Kabila hilo lilikuwa likiishi karibu na chemchem fulani iliyokuwa inajulikana kwa jina la Gamar, iliyokuwa ikipatikana kwenye njia iendayo Makka kutoka Madina. Kundi la Ukasha lilipokaribia kwa kasi kwenye chemchem hiyo ili waweze kuwazuia wasije kuleta fitina, basi hapo wakafahamu kuwa, kutokana na habari ya ujio wao kufahamika mapema, watu wa kabila lile wakawa wametawanyika. Hapo Ukasha ra na wenzake wakarudi Madina na vita ikawa haikutokea, yaani hawakupenda kujiingiza kwenye vita bila sababu yoyote. Tukio hili linabatilisha tuhuma iletwayo ya kuwa watu wale au Waislamu walikuwa wanapenda sana kupigana vita.

Katika enzi za ukhalifa wa Hadhrat Abu Bakar, Hadhrat Ukasha alikwenda pamoja na Hadhrat Khalid bin Waleed ili kuwaangamiza waasi. Isa bin Umela anasimulia kutoka kwa baba yake kwamba, Hadhrat Khalid bin Waleed alikuwa na desturi ya kwamba, akisikia adhana alikuwa hashambulii lakini kama hakusikia adhana alikuwa anashambulia.

Alipofika kwa watu hawa waliokuwepo katika eneo la BAZAAHIK, alimtuma Hadhrat Ukasha na Thabit bin Akram kama majasusi ili walete habari za maadui. Hawa wote wawili walikuwa wamepanda farasi wakati jina la farasi wa Hadhrat Ukasha lilikuwa ni Ar redhaam na jina la farasi wa Hadhrat Thabit lilikuwa ni Almahbar. Wawili hawa wakakabiliana na Tuleha na ndugu yake Salma waliokuwa wamelitangulia jeshi lao ili kupata habari za Waislamu. Tuleha akapambana na Hadhrat Ukasha na Salma akapigana na Hadhrat Thabit. Ndugu hao wawili wakawaua masahaba hawa wawili.

Abu Waqid Nesi anasimulia ya kwamba: Tulikuwa tunatembea mbele ya jeshi la wanajeshi mia mbili na tuliendelea kusimama karibu na hao wawili waliouawa hadi Hadhrat Khalid akaja na tukawazika kwa idhini ya Hadhrat Khalid wakiwa katika nguo zao zilizoloa damu. Tukio hili lilitokea mnamo mwaka 12 wa kihijiria.

Hadhrat Kharjah bin Zaid alikuwa ni sahaba wa Mtume saw. Yeye alitokana na ukoo wa Aghraz wa Khizraj. Binti ya Hadhrat Kharjah, Hadhrat Habiba alikuwa mke wa Hadhrat Abu Bakar Siddik, ambaye alimzalia Hadhrat Abu Bakar binti aitwaye Hadhrat Umme Kulthum. Mtume saw aliwafanya Hadhrat Kharjah na Hadhrat Abu Bakar wawe ndugu. Yeye alikuwa anahesabiwa miongoni mwa masahaba wakubwa. Yeye alifanya baiati katika Ukba. Wakati wa kuhamia Madina, Hadhrat Abu Bakar Siddik alikaa katika nyumba ya Hadhrat Kharjah bin Zaid.

Yeye alishiriki katika vita vya Badri na akauawa shahid katika vita vya Uhud akipigana kwa ujasiri mkubwa sana. Alikuwa na majeraha zaidi ya kumi na tatu mwilini mwake. Alipokuwa ameanguka chini kutokana na majeraha mengi, Safwan bin Umayya alimwona na kumwua na kumkata sehemu mbalimbali za mwili wake na akasema huyu ni miongoni mwa watu waliomwua baba yangu katika vita vya Badri. Sasa nimepata nafasi kuwaua marafiki bora wa Mtume Muhammad saw na kujituliza nafsi yangu. Basi yeye aliwaua Hadhrat ibne Kaukal, Hadhrat Kharjah bin Zaid na Hadhrat Aus bin Arqam.

Hadhrat Kharjah na Saad bin Rabii waliokuwa ni mtu na binamu yake, walizikwa pamoja ndani ya kaburi moja.

Imesimuliwa kuwa hadhrat Abbas bin Ubada alikuwa anasema kwa sauti kubwa siku ya Uhud kwamba: Enyi kundi la waislamu, mushikamane na Nabii wenu, msiba mlioupata mmeupata kwa ajili ya kumuasi nabii wenu. Yeye alikuwa anawaahidini msaada lakini hamkufanya subira. Kisha Abbas bin Ubada akalivua vazi lake la vita na kumuuliza hadhrat Kharjah bin Zaid kwamba: Je unalihitaji? Kharjah akajibu hapana. Ninachotaka ni kile kile ukitakacho. Kisha wote wawili wakapambana na maadui.

Abbas bin Ubada (alisikika) akisema kwamba, kama mtume saw amepata shida na taabu mbele yetu, basi tutakuwa na udhuru gani mbele ya Mungu? Na hadhrat Kharjah akasema hatutakuwa na udhuru wala hoja mbele ya Mola wetu.

Hadhrat Abbas bin Ubada aliuawa na Sufyan bin Abdu ul shmas Salmi na Kharjah bin Zaid alipata zaidi ya majeraha kumi ya mishale.

Hadhrat Malik bin Dukhsham alipita jirani ya Kharjah bin Zaid katika siku hiyo ya Uhud wakati Hadhrat Kharjah akiwa ameketi akiwa na majeraha mengi. Alipata majeraha kama kumi na tatu hivi. Hadhrat Malik akamwambia, je hujui kuwa mtume Muhammad saw ameshauawa? Hadhrat Kharjah akasema: Kama yeye ameshauawa, basi kwa yakini Allah Mtukufu yuko hai wala hatakufa. Muhammad saw ameshafikisha ujumbe, ninyi pia mpigane kwa ajili ya dini yenu.

Hadhrat Kharjah alikuwa na watoto wawili, mmoja wao alikuwa Zaid bin Kharjah aliyefariki katika zama za ukhalifa wa Hadhrat Athmani ra. Mtoto wa pili wa hadhrat Kharjah alikuwa Rabiba binti wa Kharjah aliyeolewa na hadhrat Abu Bakr Siddiq ra. Hadhrat Abu Bakri ra alipofariki, mke wake huyu Rabiba alikuwa mja mzito na wakati ule hadhrat Abu Bakri ra akasema: Natarajia kupata mtoto wa kike kutoka kwake: Hivyo yeye alizaliwa akiwa binti.

Kisha kuna swahaba mwingine wa mtume saw ambaye ni hadhrat Zyad bin Labid, jina la mama yake lilikuwa amra binte abiid bin Matruf. Hadhrat Zyad alikuwa na mtoto aitwaye Abdullah. Yeye alifika kwa mtume saw pamoja na watu 70 wakati wa baiat ya Uqba ya pili na kusilimu. Mara tu aliporudi Madina baada ya kusilimu, akayavunja masanamu ya kabila lake la bani Riaza.

Yeye mwanzoni alikuwa akiyaabudu masanamu kisha akahamia Makka kwa mtume saw na kukaa huko huko hadi mtume saw alipohamia Madina naye pia akahama pamoja na mtume saw…hivyo hadhrat Zyad anaitwa Muhajir na Ansar pia, yaani aliyehama kisha akawa pia miongoni mwa Maansar.

Hadhrat Zyad alikuwa pamoja na mtume saw katika vita vya Badr, Uhud, Khandaq na vingine vyote. Mtume saw alipofika Madina baada ya kuhamia huko na kupitia kwa ukoo wa banu Byaza, basi hadhrat Zyad alimkaribisha kwa kusema ahlan wa sahlan wa marhaba na kupendekeza Mtume saw aishi nyumbani mwake. Hapo Mtume s.a.w. akasema muacheni ngamia wangu awe huru yeye atatafuta mwenyewe pa kukaa.

Mtume saw alipowateua watu kadhaa kwa ajili ya kupokea sadaka na zaka mnamo tarehe 9 ya Muharram basi akamteua hadhrat Zyad

Endelea uk. 4

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Islamu na Malezi Bora ya Watoto

Mwl **Issa Salum Disowile**
Shule ya Sekondari Ahmadiyya

Katika dunia hii ya leo, serikali katika nchi mbali mbali zinajaribu kutunga sheria na kanuni ili kulinda jamii zao na kufanya dunia kuwa makazi salama. Bila ya hizi sheria, kanuni na miongozo watu wengi wangeingia katika migogoro na magomvi ya mara kwa mara.

Ni kweli kabisa watoto wetu na vizazi vyetu vya baadae ndiyo viongozi wa kesho, hivyo malezi bora kwao yanahitajika ili kujenga jamii yenye heshima, amani na mpagilio mzuri. Tafiti nyingi zinaonyesha kwamba malezi yana mchango mkubwa katika ustawi na maendeleo ya mtoto kiakili, kimwili, kijamii na kiroho. Na hivi ndivyo vipengele vinavyo ashiria kwamba mtoto atakuwa mtu mwajibikaji na mwenye furaha. Kwahiyo malezi bora yanahitajika ili kuilinda jamii ya baadae na kuimarisha amani katika nyumba zetu na jamii kwa ujumla.

Lengo la malezi hufanana katika nchi na jamii nyingi, tofauti huwa katika njia zinazotumika kufikia lengo hilo kulingana na mila na tamaduni zao husika. Licha ya kutofautiana katika jamii na dunia juu ya njia bora za malezi ya watoto, mafundisho ya dini ya kiislam juu ya malezi bora ya watoto hufanana diniani kote.

Imewachukua miongo mingi watafiti wa mambo ya malezi na ukuwaji wa watoto kugundua njia za malezi na hatua za ukuaji wa mtoto, cha kushangaza ni kwamba mambo haya yote wanayogundua sasa hao watafiti juu ya ukuaji na malezi ya mtoto, yalikwisha teremshwa katika Qur'an tukufu miaka zaidi ya 1400 iliyopita kupitia Mtume wetu Mtukufu Muhammad(s.a.w). Kanuni za Qur'an Tukufu zinazingatia mahitaji ya asili ya binadamu na kanuni hizo ziliteremshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kipindi ambacho hapakuwa na njia zozote za kisayansi, kisaikolojia au hata za kitabibu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Na Tumekuteremshia Kitabu kielezacho kila kitu, na mwongozo, na rehema, na habari za furaha kwa wajisalimishao."(An-Nahl: 90)

KUJIANDAA KUWA MZAZI

Katika kujiandaa kuwa mzazi watu wengi hujaribu kujiweka vizuri kiafya kwa kula mlo kamili na kuhakikisha mume na mke wanakuwa na afya njema kwasababu "malezi bora ya mtoto huanza muda mrefu kabla hata ya mimba kutungwa"

Mafundisho ya kiislamu yanaenda mbele zaidi ya haya kwa kutufundisha sisi kwamba jambo la kwanza kabisa kwa mume na mke wakati wa kujiandaa kuwa wazazi ni KUMWOMBA MWENYEZIMUNGU na kuomba wapate kizazi chema, sawa na aya hizi hapa chini:

"Mola wangu, Unipe kutoka Kwako wazao wazuri; kwa yakini Wewe ndiwe Usikiaye maombi." (Al-Imran: 39)

Na wale wanaosema: "Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu)." (Al-Furqaan: 75)



Mwl **Issa Salum Disowile**
Mwandishi wa Makala hii

Masihi aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad(as) alisema juu ya hili kwamba: "kuna maombi mengine ambayo ni ratiba yangu ya kila siku. Huwa naomba kwa ajili yangu mwenyewe kwamba Mungu aniwezeshe kufanya mambo ambayo yanaweza kuonyesha heshima na utukufu wake na Yeye(Mwenyezi Mungu) aweze kunifanya nizame katika mapenzi yake. Kisha namwomba Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mke wangu kwamba Anipe watoto kupitia yeye wanao pendezesha macho na ambao wataishi maisha yao yote kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu. Kisha ninawaombea watoto wangu kwamba Mungu awafanye wote watumishi wa dini yake"(Malfuzat, Jal. 2 uk. 4).

Ushahidi wa Qur'an kuhusiana na utungwaji wa mimba(conception) na ujauzito(pregnancy) ulioteremsha kabla ya sayansi na dawa za kisasa

Baada ya mimba kutungwa, Qur'an Tukufu inatoa mwanga juu ya hatua za ukuaji wa kiinitete (embryo), kijusi (foetus) na hatua za ukuaji wa mtoto wakati wa ujauzito:

"Na kwa yakini Tulimwumba mwanadamu katika mateuzi ya udongo. Kisha Tukamfanya mbegu katika kao lililohifadhika. Kisha Tukaiumba mbegu kuwa pande la damu, na Tukaumba pande la damu kuwa pande la nyama, kisha Tukaumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama, kisha Tukaifanya kiumbe kingine. Basi mwenye mibaraka ni Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbao." (Al-Mu'minuun: 13-15)

Katika aya hapo juu, Qur'an Tukufu inaeleza hatua tofauti za ukuaji wa mwili wa mwanadamu na hivyo kuweka uwiano mkubwa kati ya ukuaji wa kimwili na kiroho. Ukiachana na ufundi wa kibailojia, surah inatoa maelezo kwa lugha wazi na inayoeleweka. Bailojia haikugundua kitu chochote ambacho ni kinyume na kinapingana na maelezo ya Qur'an.

Maneno "tulimwumba mwanadamu katika mateuzi ya udongo" yanataja utaratibu wa uumbaji wa mwanadamu kuanzia hatua za mwanzo kabisa anapokuwa si kitu katika hali ya udongo au mavumbi na madini au virutubisho vya ardhini, ambavyo kwa kupitia michakato kadhaa ya mabadiliko, hubadilishwa na kuwa vijidudu vyenye uhai kwa njia ya chakula ambacho binadamu anakula.

Katika hatua hii Mungu anasema kwamba "mifupa tukaivika nyama" ukuaji wa kimwili wa kiinitete (embryo) huwa umekamilika.

Na maneno "kisha Tukakifanya kiumbe kingine" yanaonyesha kwamba roho haingizwi ndani ya mwili wa binadamu kutoka nje, bali huumbika ndani ya mwili wakati kiumbe kikiendelea kuumbika ndani ya mfuko wa uzazi (womb). Mwanzo huwa haina tofauti na mwili bali kupitia mabadiliko ambayo mwili hupitia wakati wa ukuaji wake ndani ya mfuko wa uzazi (womb) kitu kinachoitwa roho huumbika. Mara tu uhusiano huu kati ya mwili na roho unapokamilika moja kwa moja, moyo huanza kufanya kazi. Roho sasa huwa na sehemu yake katika mwili ambao sasa hutumika kama ganda (shell).

Qur'an Tukufu pia inasema:

"Mama yake amechukua mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu; na kumbeba na kumwachisha ziwa ni miezi thelathini; hata anapofikia balehe yake na akawa mwenye umri wa miaka arobaini, akasema: Ee Mola wangu, Uniwezeshe nishukuru neema Zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na ili nifanye vitendo vizuri Unavyovipenda, na Ukanifanyie wema katika watoto wangu; kwa yakini ninatubu Kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu.". (Al-Ahqaf: 16)

Maelezo mafupi ya Qur'an Tukufu ya tafsiri ya kiingereza yanahitimisha kwamba:

"Katika sura ya 31 aya ya 15 ya Qur'an Tukufu ilielezwa kwamba kumnyonyesha mtoto huchukua miaka miwili, lakini katika aya hii jumla ya kipindi cha ujauzito na kunyonyesha ni kama miezi thelathini ambapo imeachwa miezi sita kama kipindi cha ujauzito; na hiyo inaonekana kuwa ni kipindi ambacho mwanamke mjamzito anahisi mzigo wa mimba, mwezi wanne ni muda ambao mwanamke mjmzito anaanza kupata hisia hizo"

Wakati wa ujauzito vitu vingi huathiri maendeleo ya mtoto. Panelope Leach ni mwasaikolojia ya malezi ya watoto, anaeleza kwamba "kwa ujumla furaha na roho nzuri (good spirits) huathiri mazingira ambayo tumbo la uzazi (womb) hutoa kwa mtoto kupitia ujumbe ambao upo katika muundo wa homoni na kemikali. Kwa kweli, watoto walio tumboni wanaweza kuathirika kabisa na hisia zao za muda mrefu. Wanawake wengi wazazi ulimwenguni kote wamezungumzia juu ya watoto kuathirika na hisia zao (moods)"….

Anaongezea Zaidi, "mimba isiyo na mfadhaiko au taabu(stress-free pregnancy) ni haki ya mama na ni wajibu wa baba kwasababu ni wajibu (obligation) kwa mtoto wao." (Penelope Leach, The Essential First year (DK, 2010), 14-15)

Na ndio sababu uislam umeweka wajibu kwa baba kumhudumia mama na mtoto na kumtunza mama wakati wa ujauzito.

Tunaona hata watu wa ustawi wa jamii na serikali kwa ujumla inahamasisha wanaume kumsaidia mama mjamzito na hata kumsindikiza clinic. Hili ni fundisho la Qur'an Tukufu.

Itaendelea toleo lijalo

TANZIA

Ndugu *Ayubu Machela* wa Msongola, Dar es salaam amefariki Mwezi Mei 2018

Inna lillahi wainna ilaihi rajiun

Waziri wa Utawala Bora Asifu Islam Ahmadiyya Tanzania

Kutoka uk. 1



Seif Hassan Nakuchima

wa Serikali ya Tanganyika Sheikh Kaluta Amri Abeid ambaye alikuwa mfuasi wa Jumuiya ya Ahmadiyya.

Akitoa salamu za shukrani kwa kukaribishwa ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry alisema kuwa Jamaat Ahmadiyya imeenea nchi nyingi duniani na hapa Tanzania ipo karibu kila pembe ya nchi. Tumekuwa na uongozi thabiti chini ya kiongozi mmoja duniani ambaye kwa sasa anaishi nchini Uingereza aitwae Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba), Jamaat yetu ni ya amani na kauli mbiu yetu ni "Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote" alisema Amir Sahib.



Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry akifafanua jambo wakati wa mazungumzo na Waziri wa Utumishi na Utawala Bora ofisini kwake.

Akizungumzia kuhusu dini na siasa, Amir Sahib alimueleza Mheshimiwa Waziri kuwa Jamaat ya Ahmadiyya popote duniani hatujihusishi na siasa wala kuunga mkono Chama chochote cha siasa japokuwa imetoa fursa kwa wanajumuiya hiyo kuwa wanasiasa bila ya kuchanganya dini na siasa na hivyo kamwe sisi siyo chanzo cha kuvurugwa kwa amani popote tulipo na kuheshimu Serikali iliyopo madarakani na kutoa ushirikiano unaohitajika kwa maslahi wa wananchi wenye dini mbalimbali.

Mwishoni mwa mazungumzo hayo Amir Sahib alimkabidhi zawadi ya vitabu Mheshimiwa Waziri Mkuchika na kupiga picha ya pamoja wakiwa nje ya ofisi yake.

Watu Walio Bora Kabisa

Kutoka uk. 2

kwenye eneo la Hazar Maut. Yeye aliitoa huduma hii hadi kipindi cha Hadhrat Umar ra. Yeye alikaa (katika mji wa) Kufa baada ya kustaafu kutoka cheo hiki na kufariki kule mnamo mwaka 41 wa Hijriyya. Historia inatuelezea kuwa fitina ya kuritadi kwa watu ilipozidi na wao kukataa kutoa zaka katika zama za ukhalifa wa hadhrat Abu Bakr ra na Ashas bin Kais Kandi pia aliporitadi, basi hadhrat Zyad aliteuliwa kwa ajili ya kuondoa fitina hii. Hadhrat Zyad alipomshambulia basi akajihifadhi kwenye ngome ya Nahiir.

Hadhrat Zyad akaizunguka kwa ukali mno hadi alichukia na kutuma ujumbe kwamba nipewe Amani mimi na watu wengine tisa basi nitafungua mlango wa ngome. Hadhrat Zyad alisema nileteeni mkataba kwa maandishi nitapiga muhuri juu yake basi wakafungua mlango baada yake na mkataba ulipochunguzwa majina ya watu tisa yaliandikwa humo lakini Ashaas alisahau kuandika jina lake hivyo alipelekwa Madina pamoja na mahabusu wengine.

Kisha kuna swahaba mwingine wa Mtume saw aitwaye hadhrat Muaattib bin Ubaid, yeye alikuwa hana mtoto. Mtoto wa kaka yake, Usair bin Urwa Alikuwa mrithi wake. Hadhrat Muaattib bin Ubaid alishiriki katika vita vya Badri na Uhadi na kuuawa kuwa Shahiid siku ya Rajii. Tukio la Rajii ni tukio lile ambamo waislamu 10 waliuawa. Hadhrat Mirza Bashir Ahmad Sahib pia aliandika juu ya tukio hili kuwa siku zile zilikuwa za hatari mno kwa ajili ya waislamu na mtume saw alikuwa analetewa habari za kuhofisha kutoka katika pande zote lakini hatari kubwa zaidi ilikuwa kutoka kwa Maqureshi wa Makka ambao walikuwa wanajionesha fahari yao na ushujaa wao kutokana na vita vya Uhad, mtume saw aliandaa kikosi cha maswhaba 10 kwa ajili ya kuchunguza hatari mnamo mwaka 4 wa Hijriyya katika mwezi wa Safar na kumteua hadhrat Asim bin Thabit juu yao na kuwaamuru kuchunguza habari za Maqureshi wa Makka kwa siri na kumjulisha mtume kuhusu mipango yao na harakati zao lakini kikosi hiki ilikuwa bado hakijatoka na wakaja baadhi ya watu wa makabila ya Azli na Qara na kuomba kwa mtume saw kwamba watu wengi wa makabila yetu wanaelekea kwenye uislamu basi Utume baadhi ya watu pamoja nasi ambao watuingize katika uislam na kutupatia mafundisho yake.

Kwa kulifuata ombi lao, Mtume saw alituma pamoja nao kikosi kile kilichoandaliwa kwa ajili ya kupata habari za Maqureshi, lakini kwa hakika watu hawa walikuwa waongo kama ilivyojulikana baadaye na wakaja Madina kwa kushawishwa na Banu Lihyan ambao waliifanya hila hii kwa ajili ya kulipiza kisasi cha rais wao Sufyan bin Khalid ili Waislamu watoke nje ya Madina nao wawashambulie na Banu Lihyan walikuwa wamshaweka ngamia wengi kwa ajili ya Azli na Qara kuwa zawadi juu ya huduma yao hii. Watu hawa wadanganifu wa Azli na Qara walipofika baina ya Asfani na Makka basi wakawapasha habari hii Banu Lihyan kwa siri kwamba Waislamu wanakuja nasi basi njooni ninyi na wakaja vijana 200 wa Banu Lihyan wakiwemo 100 wapigaji wa mishale na kuwazungukia Waislamu kwenye mahali paitwapo Rajii, watu 10 wangewezaji kushindana na wanajeshi 200, na Waislamu hawa hawakuwa na mafundisho ya kuwa na woga bali mafundisho ni hivi tu kwamba kama mnakuta hali ya namna hii na kuzungukwa na watu basi mupigane nao.

Mara maswahaba hawa wakapanda juu ya mlima wa jirani na kujiandaa kwa ajili ya kupigana nao. Makafiri ambao kudanganya sio aibu kwao wakawaita kuwa mshuke chini kutoka mlimani, sisi tunafunga ahadi madhbuti nanyi kwamba hatutakuueni. Asim ra aliwajibu kwamba hatuamini ahadi yenu wala kiapo chenu nasi hatuwezi kushuka kwa dhima yenu kisha ailsema kwa kuinua uso mbinguni kwamba Ewe Mwenyezi Mungu! Unashuhudia hali yetu, umfikishie mtume wako habari yetu hii.

Basi Hadhrat Asim na wenzake wakapambana nao na wakiendelea kupigana hadi wakauawa. Walipofikia kuuawa masahaba saba na wakabakia Khubaib bin Adi, Zaid bin Dathina na sahaba mwingine, basi makafiri wakawaita washuke chini wao hawatawadhuru na chochote, kwa sababu walinuia wawakamate wakiwa hai. Ndipo waislamu wasioelewa wakadanganyika na kushuka chini. Kushuka tu maara makafiri wakawafunga na kamba za pinde zao hapo mwenzao Khubaib na Zaid hakuweza kuonesha subira, ambaye katika historia ametajwa kwa jina la Abdullah bin Tarik, naye akawaambia hii ni ahadi yenu ya kwanza mnayoivunja haijulikani hapo baadaye mtafanya nini. Abdullah akakataa kufuatana nao. Ndipo makafiri wakamkamata na kumburuza hatua kidogo, baadaye wakampiga, wakamuua na kumbwaga pale pale. Kwa kuwa kisasi chao kilikwishatimia, makafiri wakawakamata Hadhrat Khubaib na Zaid na kuwapeleka kwa Makuresh ili kuwafurahisha na kutimiza tamaa yao ya kupata fedha, wakaongozana nao kwenda Makkah. Walipofika wakawauza kwa Makuresh. Ndipo watoto wa Harith bin Amir bin Nofal wakamnunua Hadhrat Khubaib, kwa sababu Khubaib alikuwa amemuua baba yao Harith katika vita vya Badr, na Safwan bin Umaiyah akamnunua Hadhrat Zaid. Nao wote wawili pia wakauawa.

Na sahaba mwingine Hadhrat Khaled bin Bukair pia ametajwa katika masahaba wa vita vya Badr. Hadhrat Khaled, Aaqel, Aamer na Deyas wote hawa pamoja waliingia katika dini ya kiislam katika Dar ul Arqam. Hawa ndugu wanne walikuwa wa kwanza kukubali kuingia katika dini ya kiislam katika Dar ul Arqam. Mtume Muhammad (s.a.w) aliwaunganisha kuwa ndugu Hadhrat Khaled bin Bukair na Hadhrat Zaid bin Dathina. Hadhrat Khaled alikwepo katika vita vya Badr na Uhad na akauawa katika tukio la Raji' ambalo hapo kabla nimeshalieleza ambamo waislamu kumi waliuawa kwa sababu ya udanganyifu. Mtume Muhammad (s.a.w) kabla ya vita vya Badr alituma jeshi dogo likiongozwa na Hadhrat Abdulla bin Jahsh kwenda kukabiliana na msafara wa Makuresh, Hadhrat Khaled bin Bukair pia alikuwamo katika jeshi hili. Yeye aliuawa pamoja na Athim bin Thabit na Marthad bin abi Marthad Ranwi katika vita vya Raji' akipigana na watu wa makabila ya Azal na Ukara, katika mwezi wa Safr mwaka wa 4 wa Hijra akiwa katika umri wa miaka 34.

Hadhrat Masih Aliyeahidiwa (a.s) katika kitabu chake amesema: "Shukrani iwe juu ya Mwenyezi Mungu Mwenye kujaalia kheri, Afanyaye hisani na mwenye kuondoa huzuni. Na tunamsifu na kumsalia Mtume wake (s.a.w) ambaye ni imamu wa Jinn na Ins, mwenye nafsi takatifu na anayewavutia watu peponi. Na salam ziwe juu ya masahaba zake walioikimbilia chemchem ya Imani kama mwenye kiu na kung'arishwa katika ubora wa kielimu na kivitendo katika siku za giza nene la upotevu."

Anasema tena kuhusu masahaba: "Wao walikuwa simba jasiri wa wakati wa mchana wakipigana, nao walikuwa wacha Mungu nyakati za usiku (yaani walikuwa wafanyao ibada ya usiku), nao walikuwa nyota za dini zilizong'aa. Wote wanastahiki Radhi ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Atujaalie uwezo ili tuweze kufanya hali yetu ya kielimu na kivitendo iwe bora Zaidi na kuboresha viwango vya ibada zetu nyakati za usiku. Aamin.

Miongozo ya Namna ya Kumuandikia Huzur a.t.b.a Barua

Kwa hakika hakuna hata mmoja miongoni mwetu ambae asingependa kukutana na Huzur(atba), Khalifa wa Jumuiyya ya Islamu wa Ahmadiyya Duniani kote. Kama mjuavyo kumuandikia Huzur(atba) na kupata majibu yake kuna jenga hali ya Amani moyoni, mahusiano ya Kiroho na hali ya kujiamini, na jambo hili humfanya muandishi aone kama amekutana na Huzur. Hivyo kwanini tusiwe na utamaduni wa kumwandikia barua Huzur(atba) na kujenga uhusiano naye, kwa kumuomba atukumbuke katika maombi yake , na kumshirikisha katika furaha na mafanikio yetu?.

Siku zote ni vizuri Kumuandikia Huzur(atba) kwa mkono wako, na kisha utume barua yako aidha kwa Fax au Sanduku la posta. Kuna nguvu ya ziada inayopatikana ukiwa unamuandikia Barua Huzur kwa mkono wako na kuituma aidha kwa Fax au Sanduku la posta. Jambo hili linaongeza uhusiano wa karibu na Huzur(atba).

Ifuatayo ni Miongozo ya kuandika barua kwa ukamilifu kwa mpendwa wetu Huzur(atba).

1. kwa Anza na "Bismillah Rahman Rahim", inapendeza zaidi ikiwa ya lugha ya kiarabu na ikae sehemu ya juu katikati ya barua yako..
2. Andika Anuani yako, Tawi na Nchi yako pamoja na tarehe upande wa kulia wa Barua yako.
3. Anza na neno Mpendwa Huzur.
4. Baada ya hapo, toa salamu kwa Huzur " Assalamu Aleikum Warahatullah wabarakatuh"
5. Andika kichwa cha habari cha barua yako, inahusu nini. Mfano "Yah: Maombi ya Masomo yangu"
6. Mara nyingi inapendeza katika mwanzo wa barua yako, kumjulia hali Huzur(atba) hususani juu ya Afya yake na kumuombea Allah aweze kumuimarisha katika Afya yake.
7. Ni vizuri kutaja jukumu lako katika Jamaat au Tanzim na pia umuelezee Huzur ni shughuli gani unafanya kama ni Mwanafunzi au kazi nyingine yoyote.
8. Muombe Huzur, akufanyie maombi juu ya Afya yako, furaha, mafanikio au jambo lingine lolote ambalo unahitaji Huzur(atba) akuombee. Pia unaweza kumshirikisha Huzur(atba) juu ya jambo lolote linaloleta athari.
9. Kisha mtakie kheri Huzur(atba) na toa salamu ya kumuaga.
10. Andika wako mtiifu, wako katika Imani au Mwanao mpendwa wa kiroho n.k na kisha weka Saini yako na chini ya saini Andika Jina lako Kamili.
11. Jitahidi sana Barua yako iwe fupi na ielezee moja kwa moja dhumuni la barua.

ANUANI YA HUZUR(ATBA).

16 GRESSENHALL ROAD,
LONDON SW18 5QL,
UNITED KINGDOM.

FAX.

+ 011442088705234.

I s l a m n a D e m o k r a s i a



Mwl. Abdullah Hamis Mbanga
Mwandishi wa makala hii

Je, Islam inaendana na Utawala wa Kidemokrasia?

Je, Sheria ya Kiislam (Sharia) Inaweza Kugeuzwa kuwa Katiba ya Kuendeshea Serikali ya Kisiasa?

Haya ni baadhi tu ya maswali yanayoendelea kushika kasi kubwa katika miaka ya karibuni.

Watu wa magharibi hawaamini iwapo Waislamu wanao uwezo wa kuvumiliana, uwezo wa kuendesha serikali chini ya mfumo wa mitazamo tofauti ya kisisasa na kiitikadi (pluralism). Na kwamba wanayo shaka iwapo Islam yenyewe kama dini inaruhusu Waislam kuishi kwa kutangamana na watu wa Imani nyingine kwa Amani, hasa katika dola iliyo chini ya nguvu za Waislam.

Wasiwasi wote huu unatokana na kuibuka kwa nadharia inayozidi kupata mashiko kwa baadhi ya Waislam ya kwamba ili Islam isimame duniani ni lazima iwe na dola. Wapo Waislam wanaohubiri kuwa bila ya Waislam kushika dola, kamwe hawawezi kusimamisha dini sawa na matakwa ya Allah.

Hivyo kutokana na nadharia hiii, makundi mbalimbali ya wanaharakati wa kidini yameibuka duniani na kuanzisha kampeni za kufanikisha uwepo wa Dola ya Kiislam duniani. Kuna makundi yanayoendelea na ushawishi, kuna yaliyo misituni yakiendesha vita, na hata kuna ambayo tayari yamedhibiti sehemu fulani katika baadhi ya nchi yakiendesha wanachokiita dola ya Kiislam.

Kuna makundi yanayosisitiza kuanzishwa kwa Ukhalifa kuwa ndiyo suluhu pekee ya Waislam kushika dola. Harakati hizi zilianza kuenezwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, baadaye zilififia. Lakini kunako miaka ya 2010 ziliibuka tena kwa kasi kubwa. Vipeperushi vingi vilisambazwa kushawishi Waislam duniani kote kuanzisha Ukhalifa. Hizbu Tahrir ni mojawapo ya makundi yanayohubiri nadharia hii kwa nguvu kubwa.

Kuibuka upya kwa harakati hizo kuliwatisha hata baadhi ya wanahabari wa nchi za magharibi, kiasi kwamba mnamo mwezi Septemba mwaka 2011, gazeti moja maarufu la Uingereza (The Economist) lilichapisha Makala yenye kichwa cha maneno "*Dreaming of a caliphate*" (ndoto ya Ukhalifa). Katika makala hiyo mwandishi alikejeli mno madai ya wanaharakati hao kutaka kuanzisha Ukhalifa ili kushika dola. Alihitimisha kejeli zake kwa kusema Waislam hawawezi kutoa haki za kijamii na uhuru wa kiitikadi, hawawezi kukubali demokrasia na hawaungi mkono uwepo wa upinzani wa kisiasa.

Haya bila shaka ndiyo mawazo yaliyo katika mawazo ya raia wengi wa nchi za magharibi kuihusu Islam. Dhana hii imewapeleka sio tu katika kuwachukia wanaharakati hao wa Kiislam anaowaita kwa majina mbalimbali mabaya, lakini pia kuichukia Islam yenyewe kwa ujumla. Na kwa kuwa nchi hizi ni nchi zenye ushawishi mkubwa duniani, chuki hii dhidi ya Islam imeambukizwa kwa nchi nyingi zinazojihesabu kuwa zinafuata mfumo wa kidemokrasia.

Wao wanauona Ukhalifa kuwa ni kama ofisi ya mtawala wa kisiasa wa Kiislam ambaye lengo lake ni kuitawala dunia nzima kisiasa chini ya bendera ya Islam.

Dhana yao inatiwa nguvu zaidi na taarifa za kihistoria kuhusu Ukhalifa kama ule wa Umayya, Othman n.k. ambamo Makhalifa walikuwa ndio watawala wa nchi.

JE KHALIFA NI MWANASIASA?

Kuna maswali mengi yanayohitaji majibu kuhusiana na dhana hii, kwanza Ukhalifa ni nini? Ni lazima Khalifa awe na nguvu za kisiasa? Au ni mtawala na kiongozi wa kiroho tu? Na je, Islam inasemaje kuhusu serikali inayotokana na watu bila kujali imani zao za kidini? Je, katika dola ambayo Waislam ndio wenye nguvu, haki, uhuru na nafasi ya wasio Waislamu inatazamwaje? Na kwamba sharia ya Islam dhidi ya uhalifu itasimamiwaje katika nchi ambayo pia kuna watu wasio Waislamu?

Maswali haya yote yanahitaji upembuzi wa kina wa Quran Tukufu na Hadithi za Mtume s.a.w. ili kuyapatia majibu. Pia kutazama mifano katika maisha halisi ya Mtume mtukufu wa Islam s.a.w. Kiukweli ni kwamba Khalifa ni kiongozi wa kidini na kamwe si mwanasiasa. Ingawa kuna hata baadhi ya Waislam wanaoshika dhana ya kwamba Khalifa ni lazima awe kiongozi wa kisiasa. Hata hivyo hili linatokana na ufinyu wa elimu kuhusu maana na falsafa ya Ukhalifa katika Islam.

Ieleweke kuwa neon la Kiarabu 'Kalifa' humaanisha kiongozi, mrithi wa uongozi, msaidizi au mbadala. Kwa mujibu wa quran tukufu ni kwamba Khalifa huwekwa madarakani na Allah (2:31). Khalifa pia ni kiongozi anayekuja baada ya kuondoka kwa Nabii kwa lengo la kuendeleza ujumbe wa nabii huyo. Na ndiyo maana hadi sasa jitihada na harakati za baadhi ya Waislam duniani kuazimia kusimika Ukhalifa kwa juhudi zao zimegonga mwamba.

Ikumbukwe kuwa Manabii wa Allah aghalabu huwa hawaji kwa ajili ya utawala wa kimwili na kisiasa. Hawaletwi kwa ajili ya kushinda maeneo na kuanzisha dola zao, badala yake huletwa duniani kwa ajili ya kuhamasisha na kustawisha ibada ya Mungu Mmoja nakuwainua wanadamu katika madaraja ya kiroho. Quran tukufu inabainisha kwa uwazi mno majukumu ya Nabii katika aya ifuatayo:

"kama Tuivyomtuma mtume kwenu kutoka miongoni mwenu, anawasomeeni aya Zetu na kuwatakaseni na kuwafundisheni kitabu na hekima na kuwafundisha mliyokuwa hamyajui." (2:152)

ivyo malengo ya Manabii ni kuwasomea watu aya za Mwenyezi Mungu, kuwatakasa watu kwa kuwapa mabadiliko ya kiroho, kuwafundisha elimu ya kumjua Mola wao na kuwafundisha hekima na busara ili waweze kujitambua kikhulka. Na pia haya pia ndiyo majukumu ya Khalifa. Hivyo Khalifa hahitaji madaraka yoyote

Endelea uk. 8

Bustani ya Washairi

ISILAMU HIZI ZAMA JAMATI AHAMADIYA

1. Najikinga kwa Manani, kutokana na shetani
Bismillah Rahmani, rahimi mwenye hisani
Kweli nawaambieni, basi nanyi eleweni
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

2. Qadiani kutokea, hadi pande za dunia
Wengi waliizuia, mpaka sasa yaenea
Ni mkono wa Jalia, hakuna wa kupingia
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

3. Kama ilivyolandia, Maka ilippozukia
Madina kuelekea, ndipo ilipoenea
Watu waliikazia, Mola Ulilegezea
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

4. Mola Aliahidini, Kuilinda yake dini
Kama si yake Manani, mbona inashamiri
Ahadi haivunjani, ndio mana mwashindwani
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

5. Kote vita vyaenea, jihadi najivunia
Mtume hakunyanyua, upanga kushikilia
Hadi waliopotea, za kwao kuzichomoa
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

6. Ahmadiyya jumuiya, amani hijalegea
Kalamu ni jihadi, sio panga kuwaua
Vita tunapigania, amani ikidumia
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

7. Islam ni amani, tafsiri ni amani
Kwani haujabaini, muradi ulo makini
Hivi mwajua kwa nini, Islamu ndio dini?
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

8. Eti wanajisemea, Issa ye yuko kulia
Kapaa bila kufia, kwenye ardhi dunia
Qur-an yatuambia, makao ni hii dunia
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

9. Ahmadiyya jumuia misingi yazingatia
Qur-ani shuhudia, maana ya tawafia
Ni Kashmiri India, kaburi kwajionea
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

10. Mbora wa waumini, yeye yupo kaburini
Jama huyo ndiyo nani, akae huko mbinguni?
Kwani anakula nini, au ungu mwampeni?
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

11. Muhammadi kufungia, Mitume kuendelea
Nani aliwaambia, enyi watu wa bidaa
Bali kuja na sharia, na sio kutushukia
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

12. Ahmadiyya jumuia, imani imejazia
Qur-ani yatuambia, itamleta masia
Sote tukasubiria, sasa tumempokea
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

13. Katukamilia dini, hiki mwajivunieni
Munasubiria nini, Issa kuja kama nani
Sasa nielewesheni, hoja mbona mjibuni
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

14. Wakristo wawambia, christmasi si sharia
Maulidi kusherekea, pamoja wafurahia
Mbona pale mwanzoa, hii kupata tokea
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

15. Ahmadiyya jumuia, bado mi naisifia
Sherehe husherekea, ila si kwa kuzalia
Ni nini alifanyia, sisi tunaangalia
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

16. E wote muwe makini, swali nawaulizeni
Kuzaliwa ndio nini, kwa watu wa duniani?
Mwajua wafwata nini, Mitume wake Manani?
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

17. Nashusha kalamu chini, ninawaaga jamani
Tuombe kwa rahmani, Atuepushe motoni
Njia sahihi ni nini, walopita waumini
Isilamu hizi zama, Jamati Ahmadiyya

Zaid Abdallah Machombe
Mabibo - Dar es salaam

KUA UYAONE.

1. Nina anza na Rabana, yu pekee duniani
Kwa jinale Subuhana, wanamuita manani
Ninawaasa vijana, siniulize kwanini
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

2. Wazazi lihangaika, wakavipata vya kwao
Wewe pia hangaika, na upate kama wao
Usiwe unaropoka, mali si zako za kwao
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

3. Usiwe unaropoka, ukatafute vya kwako
Hapo nyumbani ondoka, usije pata anguko
Kibaya zaidi Kaka, huwapendi ndugu zako
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

4. Huwapendi ndugu zako, unawapiga makonzi
Zile mali si za kwako, unawatia majonzi
Eti zako peke yako, kiherehere kama nzi
Kudeng'a denge'ni baho, kumwande kuna uvyele.

5. Mara Baba ana hiki, mara mama ana kile
Wageni hauwataki, singizia hiki kile
Moyo umetahamaki, kutwa kucha makelele
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

6. Kila saa baba yako, mara kanunua gari
Kiumbe una vituko, jiandae na hatari
Sijefika kokoriko, kapatwa na tahayari
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

7. Kalindima alinena, vile vitu ni vya kwake
Na akarudia tena, ndio msimamo wake
Natakiwa kupambana, mpaka kieleweke
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

8. Mwisho wa Moto Majivu, kuna siku utajuta
We endeleza uvivu, kisa tu umevikuta
Usijetoka mkavu, kusubiri kwenye tuta
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

9. Wasema wazazi wafe, upate kurithi Mali
Kwanini wewe usife, tena ukafie mbali
Umekaa kama tufe, pia mekosa akili
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

10. Hausaidii kazi, upo upo tu kiumbe
Hutaki kufanya kazi, mlaini kama embe
Huwaheshimu wazazi, unawapiga vijembe
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

11. Jishughulishe kijana, utumike kama Jembe
Nenda hata karakana, pale kwa Mzee Lumbembe
Tuletee danadana, uje uone kimbembe
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

12. Dhikrillah ndio dawa, kumkumbuka Manani.
Kazi sala kama kawa, usijifanye muhuni
Lazima tuende sawa, kwa miongozo kundini
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

13. Ukianza kufa wewe, wazazi watabakia
Wadogo zako wenyewe, watapata kutulia
Ulikuwa kama mwewe, kila kitu narukia
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

14. Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
Usijivike majoho, uache kimbelembele
Huna utulivu Roho, hufai kuwekwa mbele
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

15. Nashindwa kueleweshwa, na inakuwakuwaje?
Sala unapoamshwa, unasema kwani je?
Dawa ni kufurumushwa, utajua taishije
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

16. Kama kazi saidii, we unafaida gani?
Na unafanya bidii, ya kuishi hapo ndani
Wajitia uko hai, hubadiliki kwa nini?
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

17. Na vyombo hauvioshi, pindi vinapochafuka
Haupiki kisa Moshi, ubosi umetukuka
Na unajifanya Nyoshi, muziki usiku kucha
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

18. Ubosi umetukuka, unaishi kwa wazazi
Bado una ukibaka, kitambo huachi wizi
Ujibadilishe kaka, uza hata tangawizi
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

19. Baba ana Mali nyingi!, mjeuri mtaani
Vijembe navyo kwa wingi, wakejeli majirani
Eti utajiri mwingi, watamba barabarani
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

20. Wewe jiachie tuu, kuna siku utanyoka
Kiburi si Mali kitu, ni bora ukaongoka
Hamtabaki na kitu, Manani akivitaka
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

Abdallah Kalindima

Itaendelea toleo Lijalo

Nenda mara ukirudi, Mubarak Ramadhani
Wewe kwetu ni waridi, pamba jema la uzani
Twampendeza wadudi, kuwa mbali na shetani
Mazoezi ulotupa, tuimarike imani

Mhariri

RABI TAKABALI DUA

1. Kwanza natoa salamu, kwa rijali na nisai,
Kwa jina lake Qayumu, Mola Mwenye asmai,
Naghani hii nudhumu, huku nafanya duai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

2. Tunakuomba Karimu, Allah Usiyelaghai,
Utushushie naimu, na Baraka anuai,
Utuwezeshe nidhamu, kuishika kwa uhai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

3. Ilahi Mola Dawamu, Uliyeumba samai,
Tulio kundini humu, tuepushe majidai,
Isije kutuhukumu, baiati tulobai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

4. Ya Rahmani Rahimu, Huna baba na Huzai,
Utuzishie hamu, ibada tusikinai,
Tuwe bora kwa kaumu, na maasi tuyasai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

5. Ewe mwenye Kurehemu, Twaomba yako liqai,
Waja wako mahamumu, tunatafuta shifai,
Tukinge na wadhalimu,wanotufanyia mai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

6. Laaliyu Laadhimu, manani Uliye Hai,
Endeleza kwa kudumu, ujio wa khulafai,
Wanoutilia ngumu, Allah watie nazai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

7. Ni wewe ndiye Alimu, tuepushie jinai,
Na utujaze elimu, sote tuwe ulamai,
Utufanye maasumu, daraja uturufai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

8. Ndiwe Azizu Hakimu, Sifazo hazichakai,
Tupe mahaba adhimu, ili tuwe ruhamai,
Na mbele ya mahasimu, utufanye ashudai,
Rabi takabali dua, nakuomba Rahmani.

9. Na Tumwa wetu Hashimu, Aliyeleta dhuhai,
Mpe Sala na Salamu, kwa ulufu na miai,
Ili siku ya kiyamu, atutakie shufai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani.

10. Na Masihi Muadhamu, huyu wetu Mirzai,
Mjaalie kaumu, ya wafasi hukamai,
Waifanye Islamu, iwashinde sufahai,
Rabi takabali dua, Nakuomba Rahmani

11. Hapa natua kalamu, nipelee japo chai,
Niliyoyatakalamu, ni maombi si madai,
Ninaamini Rahimu, ya vilio hakatai,
Rabi takabali dua, nakuomba Rahmani.

Na **Abdallah Hamis Mbanga (Kungwi)**
Mtwara

KWA HERI NI WETU BWANA

1. Ramadhani wetu bwana, kwa wema uliingia
Nasi tulishikamana, kwa wema kukupokea
Tlifunga kwa dhamana, kwa fadhila za Jalia
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

2. Nyoyo zilitakasika, kwa kuzileta fadhila
Na mbaya alidhikika, kimya akamba kulala
Shetani ni msifika, kwa ubaya wa mikwala
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

3. Ulimwengu hutulia, ukakunywa kama tao
Wa hii yetu dunia, yalisha majaribio
Kila mja alilia, na kumsaka kwa mbio
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

4. Usiku tulisimama, Manani kumlilia
Tulikimwomba Karima, mema kutuzidishia
Mabaya yapate koma, sote tupate tulia
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

5. Ramadhani mtajika, karibu tena mwakani
Mola wetu Msifika, Atujalie mwakani
Tufikie kwa hakika, tuyapate ya Manani
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

6. Shukurani nazitoa, kunijalia kufunga
Kwake nikaelekea, kaongeza wake mwanga
Wemawe kanitolea, na mabaya kunikinga
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

7. Kaditama nimefika, sio mwisho wa kuomba
Uyaondoe mashaka, tupate nyoyo kuwamba
Utulivu kuuweka, kama ngozi yake mamba
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Harun R. Bundala
S.L.P. 54, Tabora

Je Wajua?



Kwa Nini Samaki Huliwa Bila Kuchinjwa?

Hekima nyuma ya kutochinja samaki ni kwamba samaki waliokufa ni safi kwani hana damu (itiriri kayo) ambayo inabaki kwenye nyama kwa sababu ya kufa kwake kinyume na mifugo na wanyama wengine ambao wanapaswa kuchinjwa sawa na taratibu za Kiislamu ili waweze kuhalalishwa kula maana nyama waliokufa si safi kwa sababu wana damu inayobaki ndani ya nyama kwa kufa kwao, hivyo hawezi kuwa safi isipokuwa kwa kuchinja(wakati akiwa hai) kulingana na taratibu za Kiislamu.



Nyama "halali" ni ambayo imechinjwa kwa jina la Allah, na damu yake imetoka. Nyama "twayyib" ni iliyo safi, yenye afya na yenye kukubalika kisheria au kimaadili. Quran tukufu inaweka msisitizo mkubwa juu ya vyakula. Vilivyoharibika na kuoza vimekatazwa.

Tunatakiwa kusoma dua kabla ya kula chakula ili kuomba kupata baraka za chakula.

Si kila mwindaji au mchinjaji au mvuvi husoma dua husika kabla ya kazi, hivyo mlaji unapaswa kusoma dua kabla ya kula kupata baraka, nayo ni; ***Bismillahi wa'ala barakatillahi.***

CHEMSHA BONGO

			1 A			2 U	3 T	U	O	N	G	O	Z	E	
			L				A								
			F				W								
		5 T	A	L	A	K	A			6 J		7 M			
8 N			A				F			I		U			
I			T							B		B			
9 K	A	D	I	A	N	I				R		10 A	M	I	N
A			H							I		R			
H			11 A	B	D	12 U	S	S	13 A	L	A	A	M		14 K
						M			L			K			H
						R			A						U
			15 S	I	T	A			S						L
								16 V	I	K	T	O	R	I	A
									R						

Kwenda Kulia

2. Ihdina
5. Kuvunja agano la ndoa
9. Mji Mashariki mwaDamaskas
10. Mama wa Mtume s.a.w.
11. Muislam wa kwanza kutunukiwa Nobel kwenye Fizikia
15. Mtume s.a.w. alikuwa yatima kamili akiwa na miaka_____
16. Malkia aliyeandikiwa kitabu cha "Zawadi Kwa Kaisari"
17. Maneno baada ya nia

Kwenda Chini

1. Mama ya kitabu
3. Kuzunguka Ka'aba
4. Juzuu ya 14
6.Aliyemtokea Mtume s.a.w. pangoni
7. Amiri wa kwanza Afrika Mashariki
8. Ndoa
12. Hija katika miezi isiyo ya kuhiji
13. Sala pindi jua linapomaliza nusu ya safari yake
14. Talaka kwa mkono wa hakimu

Majibu Ya Chemsha Bongo la Toleo la Juni: *Hongereni mliopatia yote*

1. MASROOR	4. MUHAMMAD	8. RAKAA	11. AAM
1. MAKKA	5. SALAAM	9. IMAMU	12. NIA
2. RABWAH	6. ADHANA	10. RAMADHANI	13. KALAM
3. NASAHA	7. HIJA		14. RAJAB

TAFUTA MANENO

Kuna maneno 28 katika jedwali hapa chini. Yatafute kwa kuyazungushia na Penseli

B	A	L	A	M	A	K	A	U	T	H	A	R	C	D	C	N
J	K	H	K	H	H	G	Y	R	I	N	K	G	C	X	X	M
M	B	B	R	K	A	A	A	D	E	Q	K	F	T	Y	T	X
B	K	T	U	R	K	A	U	M	A	H	D	A	J	J	A	L
U	H	F	T	O	L	H	M	A	A	I	E	E	N	Z	I	Z
K	O	I	G	D	U	T	R	I	N	N	H	M	M	R	W	I
H	K	N	T	J	J	A	V	U	Z	W	I	U	A	M	H	L
A	O	R	H	I	K	I	A	U	H	A	B	E	S	H	I	Y
R	G	C	U	V	L	R	Z	F	T	P	N	M	H	U	C	A
I	H	D	R	J	I	A	C	Y	U	X	M	D	Z	K	D	S
J	A	M	I	F	B	B	F	R	A	L	I	H	A	J	H	A
T	I	K	T	R	Z	N	U	U	W	F	I	Z	K	N	F	W
M	R	J	H	M	I	H	C	M	A	P	R	G	H	C	N	A
F	I	Z	I	Z	U	K	K	H	M	Y	A	Q	E	R	Q	H
Z	N	I	M	R	O	D	I	L	K	L	J	Y	R	K	M	Y
C	K	I	Q	T	A	R	A	B	A	T	K	Y	A	L	W	I

Islam na Demokrasia

Inatoka uk. 5

ya kisiasa wala ya kiserikali kwa ajilii ya kutekeleza azma hii.

Baadhi ya watu hudai kwamba majukumu hayo hayamzuii Khalifa kuwa kiongozi wa kisiasa, wakitoa mfano kwa Mtume mtukufu s.a.w ambaye kuna wakati alikuwa kiongozi wa dini na dola.

Hapa ni vyema ikieleweka kuwa, si kwamaba ni haramu kwa Khalifa kuwa kiongozi wa dola, bali kilicho wazi ni kwamba hailazimiki kuwa kiongozi wa dola ili aweze kutekeleza matakwa ya ujumbe wake.

Ikumbukwe kwamba Mtume s..w aliishi Makka kwa miaka 13 alikuwa si kiongozi wa dola, lakini bado alikuwa ni kiongozi mkuu wa kiroho kwa Waislamu. Pia historia inaonyesha kuwa wakati wa Hadhrat Ali, nguvu na utawala wa kisiasa ulikuwa kwa Amir muawiyyah, lakini bado Hadhrat Ali r.a. aliendelea kuwaongoza Waislam katika mambo yote ya kidini.

Kuna ushahidi mwingi unaoonyesha kuwa si lazima Ukhalifa uambatane na nguvu za kisiasa.

Ni vyema ikieleweka kuwa hakuna Nabii yeyote ambaye alipewa jukumu la kupigania madaraka ya kisiasa. Sawa na maelezo ya Qurn tukufu ni kwamba Manabii hawakuwa ila watoaji wa habari njema na waonyaji (6:49). Mtume mtukufu wa Islam s.a.w. alitamkiwa waziwazi na Mola wake kuwa kazi yake iwe ni kufikisha ujumbe tu (5:100).

Matokeo ya Mtume s.a.w.kuwa kiongozi wa dola hayakuwa miongoni mwa masharti ya ujumbe wake, bali ilitokana na imani kubwa waliyokuwa nayo wananchi wa Madina juu ya vipawa vya uongozi alivyokuwa navyo.

Ni kwa sababu hii ndiyo jamii za Kiarabu zilizokuwa Madina Aus na Khazraj ambazo zilikuwa ndizo ko o kubwa kisiasa huko Madina, zilipoamua kusitisha uteuzi wa kiongozi wao abdulah bin Ubayy bin Salul kuwa mkuu wa dola yao na kumsuburi Mtume Mtukufu s.a.w. ili wamkabidhi wadhifa huo.

ISLAM NA DEMOKRASIA

Islam inasemaje kuhusu utawala wa kiserikali wa demokrasia?

Kwanza, islam ndiyo iliyoitambua ile haki ya msingi ya kidemokrasia kwamba wananchi lazima wawe na kauli juu ya utawala wa nchi wanayoishi.

"Na wale waliomwitikia Mola wao na husimamisha sala na sharia yao ni kushauriana wao kwa wao, na hutoa katika yale tuliyowaruzuku"(42:39)

Hapa panatolewa msisitizo wa serikali au utawala kupokea ushauri kutoka kwa watu. Umuhimu wa kushauriana kinchi juu ya kila jambo unawekewa mkazo. Je, huu sio msingi mkuu wa serikali ya kidemokrasia?

Hata uigaji kura wa nani awe kiongozi ni sehemu ya mashauriano baina ya dola na wananchi juu ya mtu anayefaa kuwa kiongozi. Islam inaweka miongozo ya aina mbili kwa ajili ya serikali yoyote.

Kwanza inawataka wananchi wawe na uhakika na uwezo wa mtu wanayetaka kumkabidhi amana ya uongozi.

"Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa adili; bila shaka mauidha Anayowatoleeni Allah ni mazuri sana na Allah ndiye Asikiaye, Aonaye." (4:59)

na hili ndilo fundisho la kimsingi,



kwamba mchakato wowote wa uchaguzi za kidemokrasia lazima zitangulize uadilifu, uaminifu na wema.

Kwa mujibu wa islam, mpiga kura ni mdhamini wa uongozi wan chi na hivyo atawajibika mbele ya Mola wake. Kwa hiyo hapa anaaswa kuchagua mgombea mwajibikaji na mwenye uwezo wa kubeba jukumu husika na hivyo hatakiwi kuitumia vibaya dhamana aliyopewa.

Fahamu kwamba aya haisemi kwamba Waislamu ni lazima wawachague Waislam wenzao katika uongozi, bali Waislam hapa wanatakiwa kuwakabidhi amana ya uongozi wale wanaostahiki – bila kujali dini, kabila au rangi zao.

Islam inayo sifa pekee ya kuwa dini ya kilimwengu, hivyo mafundisho yake yamezidingatia mazingira ya mifumo yote ya kijamii.Ndiyo maana katika Quran tukufu kunatajwa aina mbalimbali za mifumo ya kisiasa.

Ni ukweli ulio wazi kuwa islam haipendekezi aia fulani maalum ya mfumo wa serikali, hailaumu pia mfumo wowote wa kiutawala, ingawa kwa namana fulani mfum wa kidemokrasia huonekana kuwa ndio ulio bora zaidi, lakini hata hivyo hailaumu wala kukatza mifumo mingine kama vile ufalme, uchifu, umwinyi n.k. inachsisitiza ni kwmaba lazima wananchi wawe na kauli katika mfumo wa uendeshaji wa nchi. Hata kama mfumo wa kidikteta umepewa ridhaa ya wananchi Islam haina lawama nao.

Mwongozo wa pili wa utawala katika Islam ni kwamba serikali ni lazima iendeshe mambo yake kwa uadilifu, kwani ni serikali inayoendeshwa kwa uadilifu tu ndiyo inayoweza kuitwa kuwa ni serikali ya watu ilyoundwa na watu kwa ajili ya watu.

Uadilifu na usawa ndiyo mahitaji ya msingi kwa ajili ya ustawi wa jamii yoyote iwayo. Ndiyo maana Quran tikufu imesisitiza mara nyingi kusimamia adili katika mambo yote yanayotuhusu.

Aya niliyoitaja (4:59) haisemi kuwa Waislamu wafanye uadilifu baina yao tu bali uadilifu ufanywe kwa ajili ya watu wote, hata kama watu hao ni maadui zetu kiuchumi, kiimani au kisiasa, ni lazima watendewe kwa uadilifu.

Islam haiungi mkono ukandamizaji, ulazimishaji wala ubaguzi wa aina yeyote. Hata katika nchi ambayo walio wengi ni Waislam, wachache wasio Waslam wana haki ya kuheshimiwa imani yao. Hakuna haki ya kuwashurutisha kufuata au kuhukumiwa kwa sheria za Kiislam nje ya ridhaa yao. Quran tukufu inatambulisha msingi maalum juu ya hili isemayo:

Hakuna karaha katika dini; maadam mwongozo umeshabainika kutoka



upotevu (2:257)

Ikiwa tutaitafakari aya hii kwa kina, bila shaka tutagundua aina mbalimbali za dhuluma na unyanyasaji zinazoendeshwa katika mataifa yanayojiita ya Kiislam dhidi ya watu wa imani nyingine kuwa si sehemu bali ni kinyume kabisa na mafundisho ya Quran tukufu.

Kwa mujibu wa Quran tukufu ni kwamba tofauti za kidini zinakubalika hata katika nchi inayoongozwa na Waislam. Hili pia ni tangazo la wazi ambalo Mtume mtukufu wa Islam s.a.w. aliamrishwa kuwatangazia wasioamini kwamba kila mtu anayo haki ya kuwa na dini yake (109:7).

Islam haiungi mkono dhana ya kwamba wasiokuwa Waislam hawana haki ya kupata uongozi hata kama vipawa vya uongozi wanavyo.

Kongozi mtukufu wa jumuiya ya Waislam Waahmadiyya duniani, Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. mara nyingi hutumia kauli hii katika hotuba zake kwamba mahitaji ya serikali yenye uadilifu ni kwamba masuala ya kidini ni vyema yakatenganishwa na mambo ya utawala wa nchi, ili kwamba kila mwananchi aweze kupata haki yake.

Na hii ndiyo kanuni ya Islam, ni kanuni isiyo na ubaguzi wala upendeleo. Kimsingi ni kwamba islam inatutaka tuwe waadilifu hata kwa watu walioonyesha chuki na uadui dhidi yetu, na penginepo kutokana na uadui huo wamewahi hata kututesa. Quran tukufu inatuamrisha:

Enyi mlioamini! kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah, mtoao shahada kwa adili na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msiwe waadilifu. Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa... (5:9)

Hii ndiyo kanuni kuu ya uongozi, kwamba uadui au tofauti za mitazamo na itikadi havipaswi kuwa kizuizi cha kuwafanyia watu uadilifu kwa kuwapa amana wale wanaostahili kupewa.

Katika hali hii hakuna mfumo wowote wa utawala wa kisiasa ambao unaweza kulingana na utaratibu huu uliofundishwa na Islam.

Juu ya hili, Mtume mtukufu wa Islam, Muhammad s.a.w. alituonyesha kwa mifano hai juu ya uadilifu huu wa kutochanganya siasa na imani za kidini.

Katika Madina, kama nilivyotangulia kusema kuwa Mtume s.a.w. alitunukiwa mamlaka ya uongozi wan chi. Na uongozi wake ulipokuwa na kukubaliwa na watu wa dini mbalimbali, wakiwamo Waislamu, Wakristo na Wayahudi, hawa wote walimtambua kama mkuu wao wan chi, ngawa ukiondoa Waislam, hawa wengine hawakuamini juu ya utume wake.

Inaelezwa kuwa wakati wowote mtu alipofika kwake kwa masuala ya kiserikali na kuhitaji uamuzi juu ya jambo lake. Pamoja na kuwa kwake nabii aliyeleta sheria ya mwisho na kamilifu, bado mtume s.a.w. hakuwa akikurupuka na kutoa maamuzi au hukumu kwa mujibu wa sheria ya islam. Kila mara alimuuliza mwananchi huyo iwapo angependa suala lake liamuliwe kwa mujibu wa sheria za Kiislam, Kiyahudi au hata za Nyarubanja.

Hii ni kwa sababu tu ya kwamba

Endelea uk 11

Waahmadiyya wa Tanzania Kabla ya 1964

BUKOBA
SULEIMAN KAGUNJU
MAHMUD RUSENENE
MAHFADHA JUMA
AMRI KWEYAMBA

ARUSHA/KILIMANJARO
SHABAN SHOO
AHMAD OKASH
AMRAN ABDALLAH
IDRISA SHUMA

TANGA
SHAHA KONDO
RASHID KIHAULE
SHAABAN JUMA
HATIBU JUMA
ABDALLAH BARUWA
KHATIBU TAJIRI
MKUU CHUO
ABDALLAH SALUM
SALUM OMAR PUNZI
MTANDIFO KADIANI

UJIJI
SHEIKH KALUTA AMRI ABEID
BAKARI RASHID KAZEMA
CHIEF KALUFYA
HEMEDI FARAJI MBYANA

ZANZIBAR
YUSUB KASSAM

DAR ES SALAAM
RASHID JUMANNE ABDALLAH
KHAMIS KINGWANDE JIMPOTA
MWALIMU HASSAN
MALIK OMARI MAHAMBA
KASSIM BAINA
SALUM PUNZI
KITABU PAZI
RASHID MSABAHA



TABORA
SAIDI KAMBI
NAJIM
YUSUPH DUNIA
KHAMIS MLENZI
AHMAD SANZA KOMAGI
ATHMAN KAMBAULAYA
MASOOD KASHAGA
YASIN KHAN
MIRZA FADHIL KARIM
HASSAN (NDEKELE)
YUSUPH KAMBAULAYA
FAROOQ

MOROGORO
MUHAMMAD JUMA HIGIRO
ABDULRAHMAN MUSTAFA
ALLY RAMADHAN
CHAMCHUA MILONGE
IDDY SELEMANI JUMA
BAKARI SULAMDILA

DODOMA
HASSAN SULEIMAN TOUFIQ

RUVUMA
Mamdadi Malenga

RUFIJI
ALI ABDULHAMAN NYAMKWASU
TATU ALI
MWANAHAMISI SOTOLO
ZABIBU SUNGU
HABIBU SUNGU
MWAJUMA SUNGU
SOPHIA SUNGU
NYANDETE
SULTAN MAKUKA
SOPHIA MBUNGIRO
SEFU SUNGU MATIMBWA
OMAR MBONDE
MWINYIHIJA NGILINI
SUNGU MATIMBWA
OMAR LIHENGA
RASHID MUSA
UNGANDO
SAIDI MAILO
DHAHIL MDIWILA
SAIDI NGAKONDA
ALI NYAMKWASU
MAKAMEA MWERA
OMAR ABDALLAH MATIMBWA
MSONGORO MAGENGE
MALIKI ABDALLAH MBUNGIRO
JUMA MPITAKUNZE
SHAMTE NYENGO
ABDALLAH MCHAWI
SULTANI WAMWERA
MKOGASI
UWESU SOZIGWA
JAFARI SOZIGWA
SHAABAN MALINDA
JAFARI NYANKWASU
ATHUMANI MTINDASI KISOMA
IBRAHIM MKOGASI
KASSIM RAJABU MKOGASI
RAMADHANI NGILINI
RASHID BAKARI UNGANDO
BINTI MUSSA
MUSA UNGANDO
BAKARI UNGANDO
HARUN UNGANDO
JUMA UNGANDO
SULTAN MOHAMADI UNGANDO
ALI SALUM NDENDEKELE
MUSSA NYUMBA

NJINJO
SHEIKH SALEH MBARUK KAPILIMA
ABDALLAH AHMAD MARUNDA
HEMEDI HASSAN LIPEGEYE
ABDALLAH SALUM MNUNGU
MOHAMED SALUM MNUNGU
ALI SALUM MNUNGU
LIJUMBA MOHAMEDI MNUNGU
SAIDI MZEE MATIMBWA
HEMEDI MMAMBE
ABDALLAH ALI NG'AMBAGE
SALUM ALI NG'AMBAGE
ALI ABDALLAH LIPESA
HEMEDI A. MARUNDA
SAIDI MOHAMEDI MANORO
RAJABU CHANDE

MTWARA
SHEIKH MAHADH MUSHEWEJI
SULEIMAN JEILANI
SEIF HASAN NAKUCHIMA
MZEE NANYOU
MSHAM HASAN MTEPA
NALINGA MPUNGA
HAMISI JUMA
MZEE LILENGA
SAID KHATIBU
SAID HEMEDI
MZEE MARIWATA
MZEE ABDALLAH LEMU
ISMAIL MPUKUTILE
MZEE LISINGE
MZEE NGALOMBE
MZEE MMOTO
SALUMU YUSUFU
JUMA MUHAMMED MATOLA
SELEMAN DADI
RASHIDI SEIFU
AMRI JAILANI
MZEE DIHINJI
ISMAIL MPUKUTILE
MROPE

Kwa;

Makala
Maoni
Maswali
Ushauri

Tuandikie...



mapenziyamungu36@gmail.com
S.L.P. 376, Dar es salaam, Tanzania

HABARI KATIKA PICHA



Kamanda Mkuu wa Polisi Tabora akitoa neno katika futari iliyoandaliwa ofisini kwa Mkuu wa MKoa wa Tabora



Sheikh wa Tabora akisalimiana na mmoja wa wageni katika futari iliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora

Ijtimaa ya Khuddam Yaleta Msisimko

Na **Muhsin Abbasi Kaye** - Mabibo, Dar es salaam

Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania kwa msaada mkubwa wa Allah ilikuwa na Mkutano wake wa kila mwaka unaofahamika kwa jina la Ijtmaa, ilifanyika kuanzia tarehe 22 hadi 24 mwezi wa sita mwaka 2018 katika viunga vya Jumuiya Kitonga Jijini Dar es Salaam, ambao kimsingi unashindanisha maendeleo ya kimwili na kiroho. Katika kuelekea katika jukumu lao la



Shindano la kurusha tufe kwaKhuddam katika Ijtimaa yao 2018

kutafuta ukaribu na Allah na kuwatumikia viumbe wa Allah, Khuddam walifanya mipango maalum ya usafi wa mazingira katika Hospital ya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam, tendo lililowasisimua viongozi wa Hospitali



Shindano la usomaji wa Yassarnal Quran kwa Atfal katika Ijtimaa yao 2018

hiyo. Vijana hao wa Khuddam pia waliweza kutoa damu ili kupunguza upungufu wa damu ambayo inahitajiwa na benki ya damu ili kuwasaidia wenye mahitaji ya damu hiyo.



picha ya pamoja ya washiriki wa Ijtimaa ya Khuddam pamoja na Amir na Mbashiri Mkuu baada ya ufungaji

Kwa upande wa kiroho, Khuddam wakishirikiana na Atfal ambao ni watoto wa umri wa miaka sita hadi kumi na tano, walifanya mashindano ya usomaji wa Qur'an Tukufu, kuhifadhi Hadithi za Mtume Muhammad saw, Sala ya Kiislam, Mashairi na maswali ya papo kwa papo ambayo yaliwachangamsha wote waliohudhuria. Pia washiriki waliweza kuchangamsha mwilikwa kushiriki katika mpira wa miguu, riadha, urushaji wa tufe na mbio za baiskeli.



Shindano la Hifdh Quran kwa Khuddam katika Ijtimaa yao 2018

Washindi katika mashindano yote hayo walipewa zawadi na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry ikiwa ni ishara ya kutambua na kuthamini jitihada zao.
Aidha, Sadr Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania Ramadhan Hassan Nauja Sahib, aliwaeleza kinagaubaga waliohudhuria jitihada mbalimbali za kuleta maendeleo nchini katika kipindi cha mwaka huu. Moja ya jambo muhimu lililofanywa na Tanzeem ya Khuddam nchini Tanzania ni kuwahimiza wana khuddam kuwa na mshikamno na Khilafat kwa kukitumia kikamilifu chombo chetu cha MTA. Sadr Sahib alisema hiyo ndiyo njia pekeeya kuendeleza mshikamano na Khalifa wa Allah.
Nae Amir Sahib, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry, alikabidhiwa zawadi ikiwa ni ishara ya kutambua mchango na ushiriki wake maalum katika maendeleo ya Tanzeem na nchi kwa ujumla
Kwa msaada mkubwa wa Allah, tukio lote hilo lilivutwa na kutangazwa na vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo Cloud Media Group, Mwananchi Communication na gazeti la majira.
Na hatimaye waliagwa wale ambao sawa na umri wao wanahamia kwenye Tanzeem nyingine ya Ansarullah ambao wanaanzia miaka arobaini na zaidi.
Ni dhahiri kuwa, mwisho wa Ijtmaa hii ndiyo mwanzo wa Ijtmaa nyingine na hivyo neno letu la mwisho ni kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa Ulimwengu.



Amir sahib SHeikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa zawadi kwa mmoja wa Atfal aliyeshinda katika moja ya mashindano

Dua Muhimu za Kusomwa

Kutoka uk. 12

Unijaalie katika warithi wa Bustani za neema. (26: 84-86)

Mola wangu! Bila shaka nimedhulumu nafsi yangu, basi Unisamehe... (28:17)

Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. (66: 9)

Mola wetu, Tumeamini, basi tusamehe na turehemu nawe ndiwe mbora wa wanaorehemu. (23: 110)

Mola wetu, tumedhulumu nafsi zetu; na kama Hutusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye hasara. (7:24)

Mola wetu usituweke pamoja na watu wadhalimu. (7:48)

Mola wangu! Usiniwache peke yangu; na Wewe ndiwe Mbora wa wanaorithi. (21:90)

Sema: Mola wangu! Ukinionyesha waliyoyaahidiwa: Mola wangu! Usinijaalie katika watu wadhalimu. (23: 94-95)

Mola wetu, Umekienea kila kitu kwa rehema na elimu, basi Uwasamehe waliotubu na wakaifuata njia Yako na Uwaepushe na adhabu ya Jahanamu.

Mola wetu! na Uwaingize katika bustani za milele Ulizowaahidi, na pia waliofanya mema miongoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao; bila shaka Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

Na Uwaepushe na maovu, naye umwepushaye na maovu siku hiyo, hakika Umemrehemu; na huo ni ufaulu mkubwa. (40: 8-10)

Mola wetu, Utughofiri pamoja na ndugu zetu waliotutangulia katika imani wala Usiweke mfundo katika mioyo yetu kwa walioamini; Mola wetu, hakika Wewe ni Mpole sana, Mwenye rehema. (59:11)

Mola wangu! Unighofirie mimi na wazee wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu katika hali ya kuamini, na waaminio wanaume na waaminio wanawake; wala Usiwazidishie wadhalimu ila maangamizo! (71:29)

Mola wetu, na Utupe Uliyotuahidi kwa Mitume Wako, wala Usitufedheheshe siku ya Kiyama; bila shaka Wewe huvunji miadi. (3:195)

Wewe ndiwe Mlinzi wetu, basi tusamehe na Uturehemu, nawe ndiwe Mbora wa kughofiri. (7:156)

Mola wetu, Utuondolee adhabu ya Jahanamu, bila shaka adhabu yake ndiyo iendeleayo. (25:66)

Mola wetu, hakika sisi tumeamini, basi Utughofirie madhambi yetu, na Utuepushe na Adhabu ya Moto. (3:17)

Mola wangu, Unijaalie niwe msimamisha Sala, na wazao wangu (pia); Mola wetu, na Upokee maombi yangu. Mola wetu, Unighofirie mimi na wazazi wangu na waaminio siku ya kusimama hesabu. (14: 41-42)

Mola wangu, Uniokoe mimi na ahali zangu katika yale wanayoyafanya. (26:170)

Mola wangu, bila shaka kaumu yangu wamenikadhibisha. Basi uhukumu baina yangu na baina yao hukumu (nzuri) na Uniokoe mimi na walio pamoja nami walio waaminio. (26: 118-119)

Mola wangu, Unisaidie juu ya watu wafisadi. (29:31)

Mola wake: Kwa hakika nimeshindwa, basi Unisaidie. (54:11)

Mola wetu, Usitushike kama tukisahau au tukikosa, Mola wetu, na Usitubebeshe mzigo kama Ulivyowabebebsha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri. (2:287)

Mola wetu, tumiminie subira, na Utuimarishe miguu yetu, na Utusaidie juu ya watu makafiri. (2:251)

Mola wetu, Tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na uiimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri. (3:148)

Mola wetu! hukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu kwa haki, nawe ndiwe Mbora wa wanaohukumu. (7:90)

Mola wetu, Usitufanye jaribio kwa watu wadhalimu; Na Utuokoe kwa rehema Yako katika watu makafiri. (10: 86-87)

Ee Mola wangu, Unisaidie kwa sababu wamenikadhibisha. (23:27)

Ee Mola wangu, Unijengee nyumba Peponi karibu Yako, na Uniokoe na Firauni na matendo yake, na Uniokoe katika watu wadhalimu. (66:12)

Sasa, kuna baadhi ya maombi kutoka Ahadith (maneno ya Mtume Mtukufu (s.a.w.)).

Imesimuliwa kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.) alifundisha maombi haya, '*Ewe Mwenyezi Mungu! Unisamehe makosa yangu, unilinde na maovu ya ukosefu wangu wa maarifa, ujinga na dhulma katika masuala yangu na unilinde mimi kutoka kila madhara na maovu, ambayo wewe unayafahamu zaidi kuliko mimi mwenyewe. Ewe Mwenyezi Mungu! Unisamehe makosa yangu. Unisamehe makosa yangu yote, iwe nimeyafanya kwa kujua, au kwa kutojua au kwa namna ya utani, kwani yote hayo yamo ndani yangu. Nisamehe makosa yangu yote, ambayo tayari nimeyafanya na ambayo bado sijayafanya; yale ambayo nimeyafanya kwa siri na yale ambayo nimayafanya kwa uwazi. Wewe ni Mmoja, ndiye mwenye kusababisha watu kuendelea na kurudi nyuma Wewe pekee ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.*

Pia kuna maombi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s., maombi ambayo yanatufikisha kabisa mbele ya Mwenyezi Mungu.

"Ee Mola wa ulimwengu wote! Siwezi kutoa shukrani vya kutosha kwa ajili ya neema yako. Wewe daima umeniteremshia huruma na neema zako nyingi sana juu yangu, Unisamehe dhambi zangu nisije kuangamia. Unipe upendo wako ulio safi kabisa ndani ya moyo wangu ili niweze kupata maisha mapya na kuficha madhaifu yangu. Uniwezesha kufanya matendo ambayo yatakuridhisha Wewe. Najikinga kwa Dhati yako Takatifu dhidi ya kupata ghadhabu yako. Unionee huruma, Unionee huruma, Unionee huruma. Uniokoe kutokana na mateso ya maisha haya na maisha ya Akhera kwani kila aina ya fadhili na Baraka zimo mikononi yako. Amina "

Muendelee kuwaombea wanajamaat wote ambao wanaishi katika nchi siziso na uhuru wa kuabudu na hivyo kufanya maisha yao kuwa magumu kabisa.

Muendelee kuziombea nchi za Kiislamu ili Mwenyezi Mungu Aziokoe dhidi ya maangamizi ambayo yanazikabili.

Mwenyezi Mungu Azibariki mali na maisha ya wale ambao wanajitolea na kuchangia michango mbalimbali ya Jama'at. MTA inashika nafasi muhimu kwa ajili ya kueneza ujumbe siku hizi, Mwenyezi Mungu Awape malipo mema wafanyakazi wote wa MTA na wafanyakazi wa kujitolea na kuwawezesha kutumikia zaidi kuliko hapo kabla. Allah Mwenyezi Awaruzuku watendaji wa MTA Afrika maarifa na uelewa zaidi na kuwawezesha kuboresha mipango bora ya kueneza ujumbe wa kweli wa Uislamu katika nchi zao na kwa dunia kwa ujumla. Amin.

Islam na Demokrasia

Kutoka uk. 8

pamoja na kuwa kwake Mtume lakini pia alikuwa mkuu wa dola akisimamia haki za watu wa dini mbalimbali. Kama kuwashurutisha watu huwa chini ya hukumu ya Kiislam kama wafanyavyo baadhi ya Mamula wa leo lingekuwa ni mojawapo ya mafundisho ya Quran tukufu, Mtume s.a.w. asingetuonyesha mifano hii.

SHERIA YA KIISLAM

Kuna mashaka mengine makubwa kuhusiana na sheria ya Kiislam. Kwanza ni kwa jinsi gani sheria ya Islam inaweza kuingiliana au kutumika sambamba na sheria nyingine za kisrikali. Waislam tunaamini kuwa sheria zote zilizotajwa ndani ya Quran tukufu bila shaka zimetolewa chini ya misingi ya uadilifu. Quran tukufu inasema:

"Kwa hakika Allah Anawaamuru uadilifu, na ihsan, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na ouvu, na uasi, Anawasihini ili mpate kufahamu" (16:91)

Bila shaka kutokana na msingi wa mafundisho ya kusimama juu ya uadilifu, wema na hisani, basi hapana shaka yoyote kwamba hata sheria yake itasimama juu ya msingi huo.

Ni wazi kwamba baadhi ya sheria za Islam zinaweza kuonekana kama ni za upendeleo kwa baadhi ya macho ya nje. Mathalan tukitazama sheria inayohusu mirathi, mwananmke hupata nusu ya hisa ya mwanaume, hili huonekana kama linawabagua wanawake.

Lakini ifahamike kuwa mgawanyo huu umezingatia pia mgawanyo wa majukumu baina ya jinsia hizo mbili. Wanaume ndio wanaotakiwa kuwa wahemeaji wa malisho kwa ajili ya familia zao. Kinyume chake, wanawake wana uhuru wa kutumia hisa zote kwa matumizi yao binafsi. Mwanamke ambaye amepatiwa hisa ambaye ni nusu ya ile ya kaka yake, bado anayo haki ya kuhudumiwa na kaka yake huyo. Hivyo hisa anayopata mwanaume katika mirathi kimsingi huwa inawahusu na wanafamilia wengine ilhali hisa ya mwanamke huwa ni yake binafsi na haina mgawanyo wowote.

Kutokana na sababu hizi, Islam inaona kuwa ni jambo la uadilifu kumuongezea hisa mwanaume katika mirathi. Maana ndiye huyo huyo anayebebeshwa jukumu la kulea familia, wakiwemo dada zake, baada ya mzazi wao.

Hata hivyo Islam inatambua kuwa watu wa tamaduni nyingine hawataweza kukubaliana na hili, na ndiyo maana sheria hizo ni kwa ajili ya Waislam tu, na hivyo kwa mujibu wa Islam si sahihi kuzitumia sheria hizi juu ya wasio Waislam. Huo utakuwa si uadilifu ambao Quran tukufu imetutaka tuusimamie.

Pia kuna suala la sheria za kijinai. Vipi kuhusu adhabu mathalan ya mwizi kukatwa mkono, mzinifu kupigwa mijeledi n.k.

Haya ni mambo yanayotegemea na ujumla wa uendeshwaji wa serikali husika, lakini pia yanategemea pia imani ya mhukumiwa. Islam hailazimishi adhabu hizi kutolewa kwa waio Waislam. Maana huenda hata tafsiri ya zinaa na wizi ilivyo katika Islam ni tofauti na ilivyoelezwa katika dini zao.

Mara nyingi imesimuliwa kuwa Mtume s.a.w. kuna baadhi alikabidhi watuhumiwa wa makosa hayo waliokuwa Wayahudi kwa Makuhani wao ili wahukumiwe kwa mujibu wa imani zao.

Hii inamaanisha kuwa hata kama nchi itakuwa chini ya utawala wa Islam, bado serikali itaruhusiwa kuwa na mifumo mbalimbali ya kisheria kwa mujibu wa tamaduni na mila za jamii husika, na kwamba sheria za Islam zitawahusu waaminio tu.

Kwa ujumla, islam hailazimishi sheria zake kutumika hata kwa wasio Waislam. Serikali ya Kiislam ni ile inayowapa watu uhuru wa kuamini na kuabudu na kuwajengea mazingira wezeshi ya kutekeleza sheria na ibada za dini zao. Bila shaka huu ndio msingi mkuu wa demokrasia, nah ii ndiyo kanuni ya msingi ya serikali ya Kiislam.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAMAD-SHAWW 1439 AH | JULAI 2018 | WAFA 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat 'Salman Farsii r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Hakika Mwenyezi Mungu Yu Mwona sana, haya, mkarimu. Mtu anapoinua mikono wake Kwake, Yeye huona haya kuirudisha mitupu ikipata hasara (*Tirmidhi*).

Dua Muhimu za Kusomwa

Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Wakati akitaja umuhimu wa Ijumaa, Mtukufu Mtume (s.a.w.) alisema katika tukio moja, "Kuna muda fulani kwenye (Ijumaa), ambapo, kama Muislam atakutana nao akiwa kwenye maombi, basi chochote atakachoomba kitakubaliwa au lolote jema atakaloomba, Mwenyezi Mungu, Mtukufu Atampatia."

Kila mtu katika sala anafanya maombi kwa mujibu wa fikra zake au mahitaji yake. Pia kuna baadhi, ambao, ingawa wanasali, lakini hawana tabia ya kufanya dua maalum. Kwa kifupi wao husali na kurudia rudia maneno ya sala na huichukulia kuwa inatosha. Hawajui umuhimu wa maombi.

Hivyo, leo, katika Ijumaa hii ya mwisho ya Ramadhani, Nimeona ni vyema kusoma maombi fulani, ili wale wasio na uelewa wa kutosha waweze kuelewa umuhimu wa maombi na ili sote tuweze, kama Jumuiya, kufanya maombi yetu na dua mbele ya Mwenyezi Mungu Muweza, na kisha kwa pamoja tuombe kukubaliwa maombi haya wakati wa swala.

Sasa mimi nitasoma baadhi ya maombi ya Qur'ani tukufu na baadhi ya maombi maalum kutoka Mtume (s.a.w.). Wale ambao wanayakumbuka, basi wayasome kimya kimya pamoja nami au tuseme kwa wale ambao wanaweza, basi, kwa njia zote, wasome kimya kimya na pia waendelee kuitikia 'Ameen' kimya kimya.

Mwenyezi Mungu Mtukufu, Atukubalie maombi yetu.

SubhanAllahi wa bi hamdehi subhanAllahil Azeem. Allahumma Salli 'alaa Muhammadin wa aali Muhammad

Kwanza, kuna maombi yafuatazo ya Qurani;

Mola wetu, Utupe wema duniani na wema katika Akhera, na utulinde na adhabu ya Moto. (2: 202)

Mola wetu, tumiminie uvumilivu na Utufishe watii. ' (7:127)

Mola wetu, tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe Ishara itokayo Kwako, na Uturuzuku, kwani Wewe ni Mbora wa wanaoruzuku. (5: 115)

Mola wetu, hakika tumesikia Mwitaji anayeita kwenye imani ya kwamba Mwaminini Mola wenu. Kwa hiyo tumeamini. Kwa hiyo Mola wetu, Utusamehe madhambi yetu na Utuondolee maovu yetu na wakati wa kifo chetu Utuunganishe pamoja na watu wema. (3:194)

Mola wetu, tumeyaamini Uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi Utuandike pamoja na washuhudiao. (3:54)

Mola wetu, Usiipotoshe mioyo yetu baada ya kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu. (3:9)

Mola wangu, Unipe kutoka Kwako wazao wazuri; kwa yakini Wewe ndiwe Usikiaye maombi.(3:39)

Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu) (25:75)

Ee Mola wangu, Uniwezeshe nishukuru neema Zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na ili nifanye vitendo vizuri Unavyovipenda, na Ukanifanyie wema katika watoto wangu; kwa yakini ninatubu Kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu. (46:16)

Ee Mola wangu! Nipe (mwana) miongoni mwa watenda mema. (37: 101)

Ewe Mola wangu, mimi ni mhitaji wa heri yo yote Utakayonite-remshia. (28:25)

Ee Mola wangu, Unipe nguvu nishukuru neema Yako Uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kufanya vitendo vizuri vikupendezavyo, na Uniingize kwa rehema Zako katika watumishi Wako wema. (27:20)

Mola wangu! najikinga Kwako (Uniepushe) na wasiwasi wa mashetani. Na najikinga Kwako, Mola wangu, ili wasinihudhurie. (23: 98-99)

Ee Mola wangu, Nizidishie ilimu. (20: 115)

Mola wangu! Unipanulie moyo wangu. Na Unifanyie rahisi kazi yangu. Na ufungue kifungo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu kauli yangu. (20: 26-29)

Mola wetu, Utupe rehema kutoka Kwako, na Ututengenezee mwongozo katika jambo letu. (18:11)

Mola wangu Uniingize mwingizo mwema, na Unitoe kutoka kwema. Na Unipe nguvu kutoka Kwako isaidiayo. (17:81)

Mola wangu, Uwarehemu (wazazi wangu wawili) kama walivyonilea katika utoto. (17:25)

Mola wangu, Unipe (nguvu ya kutoa) hukumu na Uniunge pamoja na watendao mema. Na unijaalie kutajwa kwa wema katika watu wa baadaye. Na

Maonyesho ya Sabasaba Yaanza Kwa Kishindo

Na Mwandishi Wetu

Maonyesho ya 42 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yameanza katika viunga vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere jijini Dar es Salaam toka tarehe 28 mwezi wa sita mwaka 2018 ambapo yameanza kwa kasi kubwa huku Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya ikiwa ndiyo mshiriki pekee kwa miaka zaidi ya arobaini kwa upande wa watu wa dini. Banda hilo ambalo kwa miaka ya nyuma liliwahi kuwa karibu na banda la Bakwata, sasa ndiyo tegemeo kubwa kwa maonyesho ya vitabu vya dini mbalimbali, kutoa huduma ya msikiti kwa ajili ya Sala tano na kuwaruhusu watu wote wanaotaka kusali kupata huduma hiyo ndani ya banda hilo bila ya kipangamizi.

Umati mkubwa umekuwa ukitembelea banda hilo toka maonyesho kuanza na kupata wasaa wa kujipatia na kujionea mafundisho mazuri ya dini ya Islam kwa kupata vitabu na machapisho ikiwa na nakala za gazeti la Mapenzi ya Mungu.



Watu mbalimbali wakipata huduma kwenye banda la maonyesho la Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya katika viwnja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Wageni lukuki wanaofika bandani hapo hukutana na huduma nzuri ya mahubiri na mazungumzo ya dini yenye bashasha na upendo mkubwa na kuwa kivutio katika maonyesho hayo.

Huduma hiyo ambayo inatolewa bure na kwa kujitolea inaongozwa na Sadr Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania, ambaye ameweka timu makini katika kuhakikisha mahubiri yanafanyika kwa kiwango cha juu, Mwenyewe pia akiwa na Mu'utamad wamekuwa wakipatikana kwa muda mwingi bandani hapo ili kutoa huduma za kiroho kwa wahudhuriaji wa maonyesho hayo.

Wakati gazeti hili likienda mitambaoni banda letu limepata kutembelewa na wageni mbalimbali ikiwemo viongozi wa kidini na kisiasa, watu wa kawaida wa ndani nje ya nchi, pia alitembelea Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Hamis Hafidh Hassan ambapo alipata fursa kupata huduma ya vitabu vya dini toka banda hilo.

Maonyesho hayo ambayo yanatarajiwa kuhitimishwa wiki ijayo ambapo Jumuiya ya Ahmadiyya inaendelea kuwa mshiriki wa muda mrefu na pekee kutoa huduma ya dini katika maonyesho hayo na kuwakaribisha watanzania na washiriki wote kwenda kujipatia huduma za kiroho bandani hapo huku wakipata fursa ya kuangalia Muslim Televesion Ahmadiyya-Africa.